

## **THINK AND TAKE STEPS**

“Chukua vitabu, kaa chini mahali popote na uanze kujisomea” (*Get books, sit yourself down anywhere, and go to reading them yourself*).

### **ABRAHAM LINCOLN**

Kitabu hiki kimeandikwa ili kujibu vizuri maswali: Kwa nini kuna watu wamefanikiwa zaidi kuliko watu wengine? Ufanye nini unapokutana na vikwazo kwenye maisha yako?

Mbinu gani unaweza kutumia ili kujijengea uhuru wa kifadha? Jinsi gani unaweza kuchukua hatua kwa mafanikio zaidi? Ufanye nini unapobaki peke yako? Mbinu gani unaweza kuitumia ili kukataa kukataliwa na watu?

Hivi unajua kuwa wewe ni mtu mkuu? Pamoja na mengine mengi utajifunza pia jinsi ya kufuata sauti yako ya ndani kipindi unapotaka kufanya maamuzi.

Mamia ya watu waliofanikiwa ambao nimekuwa nikiwahoji ili kupata jibu zuri la swali langu la msingi “**KWANINI MAFANIKIO?** Karibia kila mtu aliyefanikiwa aliniambia kuwa “*sikuwa mtu mwenye kipaji au talanta kubwa zaidi katika maisha yangu, lakini nilichagua kuamini kuwa chochote kinawezekana, nilisoma, nilifanya mazoezi na kufanya kazi kwa bidii na busara kuliko wengine na ndivyo nilivyofika hapa nilipo leo*”

Kupitia kitabu hiki utagundua kuwa, uwezo wa akili

yako kufanya kazi yenyе tija inahitaji matengenezo endelevu, misuli ya akili hudhoofika pale inapokosa matengenezo endelevu, kumbuka kuwa akili ni kama palachute inafanya kazi tu wakati iko wazi.

### **HENRY FORD,**

*“aliwahi kusema Yeyote anayeacha kusoma au kujifunza ni mzee, iwe ana umri wa miaka ishirini au themanini. Mtu yeyote ambaye anaendelea Kujifunza atabaki kuwa kijana”* (Anyone who stops learning is old, whether at twenty or eighty. Anyone who keeps learning stays young).

Ili kubaki juu, lazima ubadilike na uendelee kujifunza, hauwezi kudhani tu kwamba umemaliza kusoma mara baada ya kumaliza shule au chuo kwa sababu elimu haina mwisho, daima unahitaji kujifunza mada mpya kila hatua ili kufikia kilele cha mafanikio yako, hauna budi kuboresha ujuzi wako ambaao tayari unao.

Katika harakati za kuboresha ujuzi wako ninakukumbusha kuwa, hakuna mtu ambaye ana kinga ya kufanya makosa na kuwa na siku mbaya.

Kutakuwa na wakati ambaao hisia zako zitakushinda, kuna wakati ambaao utaamini mawazo ambayo hayako sawa, nyakati ambazo utashiriki katika tabia ya kujiharibu au isiyo na tija.

Lakini nyakati hizo zitakuwa chache na hafifu katika wakati ambaao unafanya kazi kwa bidii ili kuongeza nguvu zako za mafanikio.

**Roger Crawford**, aliwahi kusema “*kupingwa ni jambo ambalo haliepukiki, kushindwa ni hiari*” (*being challenged in life is inevitable, being defeated is optional*).

Kama kocha yejote mzuri anapaswa kutoa msaada na ushauri kukusaidia ili uwe mchezaji bora, kuwa tayari kufanya hivyo mwenyewe kupitia kitabu hiki.

Angalia kile kitu unachokifanya vizuri na uwekeze nguvu zako pale, anzia hapo kupanda ngazi ili kufikia kilele cha mafanikio yako.

**Martin Luther King Jr**, Aliwahi kusema “*Ikiwa huwezi kuruka basi kimbia, ikiwa huwezi kukimbia basi tembea, ikiwa huwezi kutembea basi tambaa, lakini hakikisha kuwa, chochote unachofanya lazima uendelee kusonga mbele*” (*If you can't fly then run, if you can't run then walk, if you can't walk then crawl, but whatever you do have to keep moving forward*).

Tambua maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa, jipe changamoto mwenyewe ili kupata matokeo mazuri na utengeneza fursa za ukuaji. **T.D.Jakes** aliwahi kusema “*Ikiwa daima utaendelea kufanya kile ambacho unafanya kila wakati, daima utabaki kuwa mahali ulipokuwa siku zote*” (*If you always do what you've always done, you'll always be where you've always been*).

Unaposoma kitabu hiki, nakuhimiza kupigia mstari na kuangazia kila kitu ambacho unahisi kuwa

muhimu kwako, weka alama kwenye mambo yote unayohitaji kuchukua hatua, jikumbushe mwenyewe kuhusu kile unachohitaji kutoka pale ulipo na unapotaka kwenda.

Kumbuka kuwa kujifunza kwa kweli hutokea tu pale unapopata taarifa mpya na kuzitumia taarifa hizo kubadilisha tabia, mienendo na muonekano wako.

Unaweza kuhisi kuchanganyikiwa kwa kutojua juu ya mambo yaliyomo ndani ya kitabu hiki, unaweza kuwa na hasira kwa wazazi na walimu wako kwa kutokulishwa mambo haya muhimu nyumbani na shulenii au hasira juu yako mwenyewe.

Kwa kuwa tayari umejifunza mengi ya mambo haya lakini hukuyafanya kazi, pumua na utambue kuwa hii yote ni mchakato wa safari yako, tambua kuwa, huu ni wakati wa kuanza kuishi maisha ya ndoto zako.

Karibu tujifunze pamoja hadi mwisho wa kitabu hiki.

**ABRAHAM LINCOLN** aliwahi kusema “*Weka miguu yako mahali sahihi kisha simama imara* (*Put your feet in the right place, then stand firm*)